# MUHULA WA PILI.

## GREDI YA TATU.

| WIKI | KIPINDI | MADA. | MADA NDOGO. | MATOKEO MAALUM YANAYOTOKEA. | MASWALI DADISI. | MAPENDEKEZO YA SHUGLI ZA UFUNZAJI | KAZI YA ZIADA. | NYEZO | MAONI. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua picha za watu na kazi mbalimbali ili kuimarisha ufahamu wa hadithi<br>● kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha usomaji na usikivu | Unaona nini kwenye picha? | Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br><br>Wanafunzi waweza kusoma katika darasa, wakiwa wawili na baadaye mwanafunzi asome peke yake. | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakielezea wanachoona kwa picha. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 62-63 | |
| | 2 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusoma hadithi kuhusu kazi mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusomakufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa | Ni aina gani ya kazi ambayo imewasilishwa kwenye picha? | Wanafunzi waweza kusoma katika darasa, wakiwa wawili na baadaye mwanafunzi asome peke yake.<br><br>Mwanafunzi anaweza kusikiliza hadithi ikisomwa kupitia | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakiimarisha stadi ya kusoma huku wakisoma hadithi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 63-64 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kuhusu kazi mbalimbali ili kupata ujumbe<br>● kuchangamkia kusoma hadithi. | | vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi na projekta.<br><br>Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa. | | | |
| | 3 | Kuandika. | Kusikiliza na kuzungumza. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi. | Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa? | Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br><br>Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br><br>Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa. | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakijadili mambo ya kuzingatia wanapoandika kisa. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 64 | |
| 2 | 1 | Kuandika. | Kusikiliza na kuzungumza. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | Je, unaweza kuandika kisa gani kifupi kinachohusiana na kazi yoyote? | Wanafunzi waweza wakaandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br><br>Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | Mwalimu awaangalie wanafunzi wakiandika kisa chochote wanachokifahamu. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 65 | |
| | 2 | Sarufi. | Ukanusho wa nyakati. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze; | Unafanya nini sasa? | Wanafunzi watumie -li-; -na-; -ta- | Mwalimu awasikilize | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | • kutambua ukanusho wa -li-; -na-; -ta- katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>• kusoma ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kuimarisha usomaji | Ulifanya nini jana? | kuelezea vitendo walivyofanya katika wakati uliopita (LI), ulipo (NA) na ujao (TA) wakiwa katika vikundi au wawili wawili.<br><br>Mwanafunzi akamilishe vifungu kwa kutumia -li-; -na-; ta- na ukanusho wake.<br><br>Mwanafunzi asome vifungu vyenye matumizi -li-; -na-; ta- na ukanusho wake. | wanafunzi wakijieleza. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 66 | |
| | 3 | Sarufi. | Ukanusho wa nyakati. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>• kuandika ukanusho wa nyakati katika sentensi ili kujenga ubunifu<br>• kuchangamkia matumizi ya nyakati katika mawasiliano. | Utafanya nini kesho?<br><br>Je, ni nyakati zipi ambazo unajua kukanusha? | Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la ukanusho wa nyakati akiwa peke yake, wawili wawili au katika kikundi.<br><br>Mwanafunzi aweza kutazama jinsi nyakati zinavyokanushwa katika vifaa vya kiteknolojia na kufanyia zoezi kwenye mtandao. | Mwalimu awaangalie wanafunzi wakiandika ukanusho wa nyakakati katika mawasiliano. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 67 | |
| 3 | 1 | Usalam a. | Msamiati. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>• kutambua msamiati ambao hutumiwa katika usalama ili kuimarisha mawasiliano | Je,ni nini maana usalama? | Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno. | Mwalimu asikize maoni ya wanafunzi kuhusu usalama. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 69-70 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | • kusoma msamiati unaohusiana na usalama ili kujenga usomaji bora<br>• kueleza maana ya msamiati wa usalama ili kuimarisha ufahamu | | Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati wa usalama akiwa peke yake au katika vikundi.<br><br>Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa usalama. | | | |
| | 2 | Usalam a. | Msamiati. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>• kutumia msamiati wa usalama katika sentensi ili kuimarisha ufahamu<br>• kuandika maneno yanayohusiana na usalama ili kujenga uandishi bora<br>• kuthamini usalama katika mazingira yake. | Usalama huhusisha mambo yapi? | Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usalama k.m. utekaji nyara na moto na kisha kujadili jinsi ya kujilinda kutokana na hatari.<br><br>Mwanafunzi atazame michoro na picha inayolenga maana ya maneno kuhusu usalama.<br><br>Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa usalama. | Mwalimu asikilize sentensi za wanafunzi kuhusu usalama. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 71-73 | |
| | 3 | Kusikili za na Kuzung umza: | Maagano. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweza:<br>• kutambua maneno yanayotumiwa katika maagano ili kuwezesha mazungumzo<br>• kutumia maneno yanayotumiwa katika maagano | Je, ulipoagana na mzazi asubuhi alikwambiaje? | Mwanafunzi anaweza kueleza matumizi ya maagano kama vile: kwaheri; siku njema, mchana mwema, safiri salama na usiku mwema.<br><br>Mwanafunzi atazame michoro inayoashiria vitendo vya kuagana. | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakiagana huku wakitumia maneno wanayojua. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 73 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kwenye mawasiliano | | Mwanafunzi ashiriki katika maigizo ya kuagana. | | | |
| 4 | 1 | Kusikiliza na Kuzungumza: | Maagano. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kujibu maagano kwa njia ifaayo ili kudhihirisha ufahamu<br>● kuthamini matumizi ya maagano katika mawasiliano ya kila siku. | Je, mzazi hukwambiaje unapoenda kulala?<br><br>Mtu anaposafiri anaambiwaje? | Mwanafunzi aweza kutazama vibonzo katika tarakilishi vikiigiza vitendo na maneno mbalimbali ya kuagana.<br><br>Mwanafunzi aweza kutaja neno la kuagana linalofaa kutokana na maelezo mbalimbali akiwa peke yake, wawili wawili au katika vikundi. | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakijibu maagano. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 74 | |
| | 2 | Kusikiliza na Kuzungumza. | Masimulizi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua mambo yanayoathiri usalama ili kujihakikishia usalama<br>● kutambua njia za kudumisha usalama katika mazingira yake ili kujihakikishia usalama<br>● kusimulia kuhusu mambo yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake ili | Usalama ni nini?<br><br>Usalama unatusaidia na nini? | Mwanafunzi asimulie baadhi ya mambo. yanayoweza kuhatarisha usalama katika mazingira yake kupitia k.m. mgeni mwalikwa.<br><br>Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake.<br><br>Wanafunzi wajadiliane namna ya kuepuka dhuluma k.m. kutozungumza na watu wasiowajua, | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakielezea maana ya usalama. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 74 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kuimarisha stadi ya kuzungumza | | kupiga ukelele anapokumbwa na hatari. | | | |
| | 3 | Kusikiliza na Kuzungumza. | Masimulizi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusikiliza masimulizi kuhusu usalama ili kujenga stadi ya kusikiliza<br>● kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku. | Unaweza ukafanya nini unapovamiwa? | Mwanafunzi aandike baadhi ya mambo yanayoathiri usalama katika mazingira yake.<br><br>Mwanafunzi asimulie kisa alichokishuhudia kuhusu usalama. | Mwalimu asikize maoni ya wanafunzi kuhusu vile wanaeza fanya wanapovamiwa. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 75 | |
| 5 | 1 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua picha zinazoonyesha usalama katika mazingira mbalimbali ili kurahisisha ufahamu<br>● kutambua maneno yanayohusiana na usalama ili kuyatumia katika mawasiliano<br>● kusikiliza hadithi za mwalimu kuhusu usalama ili kuimarisha ufahamu | Je, usalama unahusu nini?<br><br>Ukosefu wa salama husababishwa na nini? | Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi<br><br>Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi asome darasani, wakiwa wawili na baadaye asome peke yake.<br><br>Wanafunzi wasomeana hadithi wakiwa wawili wawili au katika vikundi | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakitambua picha katika kitabu. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 76 | |
| | 2 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: | Unapojipata kwenye hatari | Mwanafunzi athibitishe utabiri | Mwalimu asikilize | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | <ul><li>kusoma hadithi kuhusu usalama ili kujenga usikivu</li><li>kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu usalama ili kupata ujumbe</li><li>Kuthamini umuhimu wa usalama katika maisha ya kila siku.</li></ul> | unafaa kufanya nini? | wake baada ya kusoma hadithi.<br><br>Mwanafunzi aweza kusimulia hadithi kutokana na picha alizopewa kuhusu usalama.<br><br>Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa.<br><br>Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na hadithi. | maoni ya wanafunzi kuusu vile wanavyofany a wanapojipata kwa hatari. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 77 | |
| | 3 | Kuandik a. | Kusikiliza na kuzungumza. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<ul><li>kutambua kisa chenye mtiririko</li><li>kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada</li></ul> | Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa? | Mwanafunzi aweza kupewa hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br><br>Mwanafunzi aongozwe kujadili yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k. | Mwalimu asikilize maoni ya mwanafunzi kuhusu mambo anayofaa kuzingatia kuhusu kisa. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 79 | |
| 6 | 1 | Kuandik a. | Kusikiliza na kuzungumza. | <ul><li>Kufurahia uandishi wa visa tofauti maishani.</li></ul> | Je, unaweza kuandika kisa gani kifupi kinachohusian a na usalama? | Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili.<br><br>Mwanafunzi apewe fursa ya kuandika kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za | Mwalimu kuangalia visa mbalimbali wanafaunzi wanavyiandik a darasani. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 80 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | | | |
| | 2 | Sarufi: | Vinyume vya vitendo. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>● kutaja vinyume vya vitendo<br>● kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo | Je, unajua vinyume vya vitendo unavyofanya kila siku? | Mwanafunzi aweza kufafanuliwa juu ya vinyume vya vitendo kama vile lala-amka; keti- simama; cheka-lia; tabasamu – nuna; enda-rudi; panda – shuka nk.<br><br>Wanafunzi waweza kuigiza vinyume vya vitendo wakiwa wawili wawili. | Mwalimu apewe maana ya kinyume na wanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 80 | |
| | 3 | Sarufi: | Vinyume vya vitendo. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kuandika vinyume vya vitendo<br>● kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | Je, unajua vinyume vya vitendo unavyofanya kila siku? | Mwanafunzi aweza kushirikishwa kutunga na kusoma sentensi zilizo na vinyume vya vitendo.<br><br>Mwanafunzi aweza kuelekezwa kuandika vinyume vya vitendo. | Mwalimu awasikilize wanafunzi wakisema vinyume vya vitendo wanavyofanya kila siku. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 82-83 | |
| 7 | 1 | Usafi wa Mazingira. | Msamiati | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua msamiati wa usafi wa mazingira<br>● kutumia msamiati wa usafi wa mazingira katika sentensi | Je, unajua msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira? | Mwanafunzi aweza kuelekezwa kusoma maneno yanayohusiana na usalama kwa kutumia kadi za maneno.<br><br>Mwanafunzi aweza kuelekezwa kutoa maana ya msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira. | Mwalimu asikilize baadhi ya msamiati wa usafi kutoka kwa mwanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 84-85 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu maana za maneno yanayohusiana na usafi wa mazingira.<br><br>Mwanafunzi aweza kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na usafi wa mazingira. | | | |
| | 2 | Usafi wa Mazingira. | Msamiati | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kubainisha mazingira safi na yale machafu<br>● kuthamini mazingira safi. | Unaweza kutumia msamiati gani unaohusiana na usafi wa mazingira sentensi?<br><br>Mazingira safi ni yapi? | Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu usafi wa mazingira k.m. kuokota na kuchoma taka, kufyeka nyasi n.k.<br><br>Mwanafunzi aweza kutazama michoro na picha zinazolenga maana ya maneno kuhusu usafi wa mazingira.<br><br>Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu umuhimu wa usafi wa mazingira wakiwa kwenye vikundi. | Mwalimu asikilize maoni ya wanafunzi kuhusu mazingira machafu. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 86-87 | |
| | 3 | Kusikiliza na Kuzungumza: | Masimulizi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutofautisha mazingira safi na yasiyo safi | Ni nini maana ya mazingira?<br><br>Mazingira safi ni yapi? | Mwanafunzi aweza kufahamu maana ya usafi wa mazingira.<br><br>Wanafunzi waongozwe katika | Mwalimu asikilize tofauti kati ya mazingira chafu na safi | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 88 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ● kutambua umuhimu wa mazingira safi | | vikundi kusimulia visa vinavyohusiana na usafi wa mazingira k.v. umuhimu na jinsi ya kutunza mazingira | kutoka kwa wanafunzi. | | |
| 8 | 1 | Kusikiliza na Kuzungumza: | Masimulizi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusikiliza masimulizi kuhusu usafi wa mazingira<br>● kuelezea kuhusu usafi wa mazingira | Je, tunawezaje kuborasha mazingira? | Mwanafunzi aweza kuigiza jinsi ya kudumisha usafi katika mazingira yake<br><br>Wanafunzi waweza kutazama video inayohusu mazingira safi na chafu kisha wabainishe mazingira | Mwalimu asikilize jinsi ya kuboresha mazingira kutojka kwa wanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 89-90 | |
| | 2 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>● kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi<br>● kusikiliza mwalimu kwa makini anaposoma hadithi kuhusu usafi wa mazingira<br>● kusoma hadithi kuhusu mazingira safi | Je, unaweza kukumbuka hadithi gani uliyosoma? | Mwanafunzi aweza kujadili kuhusu picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br><br>Mwanafunzi aweza kuthibitisha utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br><br>Mwanafunzi aweza kufahamu matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi. | Mwalimu asikilize maoni ya mwanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi Kusoma: Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 91-92 | |
| | 3 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kufahamu hadithi aliyosoma na | Je, hadithi unayoweza kukumbuka inahusu nini? | Wanafunzi waweza kusoma kama darasa, wakiwa wawili na | Mwalimu asikilize wanafunzi wakihadithi | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | aliyosomewa kuhusu usafi wa mazingira<br>● kuthamini mazingira safi. | Je, umeweza kusoma hadithi ngapi? | baadaye asome peke yake.<br><br>Mwanafunzi aweza kutoa muhtasari wa hadithi aliyosoma au kusomewa.<br><br>Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi katika kundi la wawili wawili au darasa zima.<br><br>Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili. | hadithi waliyposomewa. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 93-94 | |
| 9 | 1 | Kuandika. | Kusikiliza na kuzungumza. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi. | Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa? | Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br><br>Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi kama vile mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br><br>Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi | Mwalimu asikilize mambo ya kuzingatia unapoandika kisa kutoka kwa wanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 94 | |
| | 2 | Kuandika. | Kusikiliza na kuzungumza. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kufurahia uandishi wa visa tofauti ili | Je, unaweza kuandika kisa kifupi kinachohusian | Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa wawili wawili. | Mwalimu asikilize maoni ya | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kuimarisha mawasiliano andishi. | a na usafi wa mazingira? | Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | wanafunzi kuhusu visa. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 95 | |
| | 3 | Sarufi: | Matumizi ya haraka na polepole. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua matumizi ya haraka na polepole ili kuimarisha mawasiliano mwafaka<br>● kutumia haraka na polepole katika kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano mwafaka | Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu alivyofanya jambo? | Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia haraka na polepole.<br><br>Mwanafunzi aweza kubainisha matumizi ya vielezi vya jinsi vinavyofunzwa kwa kutumia vifaa vya kiteknolojia.<br><br>Mwanafunzi atazame vitu mbalimbali na avirejelee kwa kutumia haraka na polepole k.m Mtoto anatembea polepole. | Mwalimu awatazame wanafunzi wakifanya vitu kwa haraka na polepole. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 95 | |
| 10 | 1 | Sarufi: | Matumizi ya haraka na polepole. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusoma sentensi zilizo na matumizi ya haraka na polepole ili kujenga usomaji bora. | Unatumia maneno gani kuelezea namna mtu anavyotembea? | Wanafunzi washiriki katika maigizo wakitumia haraka na polepole wakiwa darasani.<br><br>Mwanafunzi aandike maneno na sentensi kwa kutumia haraka na polepole | Mwalimu asikilize wanafunzi wakieleza jinsi wenzao wanavyotembea kwa haraka au polepole. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 96-97 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2 | Dukani. | Msamiati. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze<br>● kutambua msamiati wa dukani ili kuutumia katika mawasiliano<br>● kusoma maneno yanayohusiana na shughuli za dukani ili kujenga usomaji bora<br>● kueleza maana ya msamiati wa dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza | Mtu anayenunua kitu dukani huitwaje?<br><br>Mtu anayeuza dukani huitwaje? | Mwanafunzi asome maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia kadi za maneno kama vile nunua, uza, bei, kilo, mnunuzi, mwuzaji, hasara, faida, pesa, baki, sarafu na noti.<br><br>Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano kuhusu maana ya maneno yanayohusiana na shughuli za dukani kwa kutumia picha au michoro. | Mwalimu asikilize msamiati wa dukani kutoka kwa wanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 98-99 | |
| | 3 | Dukani. | Msamiati | ● kutumia msamiati wa dukani katika sentensi sahihi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>● kuandika maneno yanayohusiana na uuzaji na ununuzi ili kuimarisha stadi ya kusoma | Pesa unazorudishiwa unaponunua kitu dukani huitwaje? | Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati wa dukani.<br><br>Mwanafunzi aweza kutazama video kuhusu uuzaji na ununuzi.<br><br>Wanafunzi washiriki katika majadiliano kuhusu umuhimu wa kufanya biashara wakiwa kwenye vikundi. | Mwalimu asikilize wanafunzi wakitumia msamiati wa dakuni. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 100 | |
| 11 | 1 | Kusikiliza na Kuzungumza: | Masimulizi | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua maneno yanayotumiwa | Je, umewahi kununua nini dukani? | Mwanafunzi asimulie kuhusu shughuli za dukani. | Mwalimu asikilize maoni ya msamiati wa | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | katika muktadha wa dukani ili kuimarisha ufahamu<br>● kueleza shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kuzungumza | | Mwanafunzi aweza kumsikiliza mgeni mwalikwa anapotoa wasilisho lake kuhusu shughuli za dukani.<br><br>Mwanafunzi atambue maneno yanayotumiwa katika muktadha wa dukani kama vile, uuzaji, bei, kilo, ununuzi, hasara, faida, pesa na baki.<br><br>Mwanafunzi asikilize kwa makini hadithi zinazosimuliwa kuhusu muktadha wa dukani kwa kutumia maneno. | wanafunzi kuhusu dukani. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 101 | |
| | 2 | Kusikiliza na Kuzungumza: | Masimulizi | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusikiliza masimulizi kuhusu uuzaji na ununuzi ili kujenga usikivu<br>● kuthamini biashara katika maisha ya kila siku. | Je, ulitumia kiasi gani cha pesa kununua ulichotumwa? | Mwanafunzi aweza kutazama video inayoonyesha mambo yanayohusiana na ununuzi na uuzaji dukani.<br><br>Mwanafunzi ashiriki katika mjadala kuhusu shughuli za dukani katika vikundi.<br><br>Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kuhusu shughuli za dukani. | Mwalimu asikie maoni kutoka kwa wanafunzi kuhusu kiasi cha pesa walichowahi kutumia dukani. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 102-103 | |
| | 3 | Kusoma: | Hadithi. | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kutambua msamiati uliotumiwa katika | Umewahi kusoma hadithi gani | Mwanafunzi asikilize mwalimu akisoma hadithi ya mwalimu | Mwalimu asikilize wanafunzi wakitumia | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | hadithi ili kuwezesha ufahamu<br>● kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu kuhusu shughuli za dukani ili kuimarisha stadi ya kusikiliza | kuhusu dukani? | na baadaye kuuliza na kujibu maswali.<br><br>Mwanafunzi asome pamoja na wengine darasani, kisha wasome wawili wawili na baadaye asome peke yake.<br><br>Mwanafunzi ajadili picha kwenye hadithi. | baadhi ya msamiati kutunga sentensi. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 104 | |
| 12 | 1 | Kusoma: | Hadithi | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kusoma hadithi kuhusu dukani kwa ufasaha ili kujenga usomaji bora<br>● kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu shughuli za dukani ili kupata ujumbe | Umewahi kusoma hadithi gani kuhusu dukani?<br><br>Je, ni hadithi gani iliyokufurahisha zaidi? | Mwanafunzi atabiri kuhusu kitakachotokea katika hadithi wakiwa wawili wawili.<br><br>Mwanafunzi ashirikiane na wengine kujadili msamiati uliotumika katika hadithi.<br><br>Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi husika ikisomwa | Mwalimu aeleze hadithi yoyote alioisoma. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 105 | |
| | 2 | Kusoma. | Hadithi | ● kuthamini biashara maishani kama njia moja ya kujitegemea maishani. | Umewahi kusoma hadithi gani kuhusu dukani?<br><br>Je, ni hadithi gani iliyokufurahisha zaidi? | Wanafunzi waweza kusomeana hadithi katika vikundi.<br><br>Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi aliyosoma<br><br>Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali. | Mwalimu asikilize maoni ya wanafunzi kuhusu hadithi iliyowafurahisha. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 106 | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Mwanafunzi ashiriki kujadili baadhi ya maswali darasani, katika vikundi au wakiwa wawili wawili. | | | |
| | 3 | Kusikilizа na kuzungumza. | Kuandika | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>● kuandika kisa kifupi kwa hati nadhifu kulingana na mada ili kujenga stadi ya uandishi | Je, ni mambo yapi yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa? | Mwanafunzi apewe hadithi yenye mapengo ajaze kwa maneno mwafaka.<br><br>Mwanafunzi aeleze yaliyo muhimu katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.<br><br>Mwanafunzi asome kielelezo cha kisa kilichoandikwa na mwanafunzi. | Mwalimu asikilize mambo yanayofaa kuzingatiwa unapoandika kisa kutoka kwa wanafunzi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 106 | |
| 13 | 1 | Kusikiliza na kuzungumza. | Kuandika | ● kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | Je, ni mambo gani utakayoshughuliki a katika ukiandika kuhusu dukani? | Wanafunzi waweza kuandika kisa kifupi wakiwa Wawili wawili.<br><br>Mwanafunzi aandike kisa kifupi kinachohusiana na mada. Kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. | Mwalimu asikilize kutoka kwa wanafunzi mambo ya kuzingatia unapoandika kuhusu duka. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 107 | |
| | 2 | Sarufi. | Matumizi ya alama ya kuuliza(?) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze: | Je, alama (?) huitwaje? | Mwanafunzi aandike alama ya kuuliza (?). | Mwalimu asikize baadhi ya | Mwanafunzi Tarakilishi | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | • kutambua matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika kuimarisha mawasiliano | | Mwanafunzi afafanue matumizi ya alama ya kuuliza (?). | matumizi ya kiulizi kutoka kwa wanafunzi. | Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 108-109 | |
| | 3 | Sarufi. | Matumizi ya alama ya kuuliza(?) | • kusoma sentensi zilizo na matumizi ya alama ya kuuliza (?) katika | Je, utatumia alama (?) unapofanya nini? | Mwanafunzi atunge sentensi akitumia alama ya kuuliza (?).<br>Mwanafunzi asome sentensi zilizo na alama ya kuuliza (?). | Mwalimu atazame baadhi ya sentensi wanafunzi wameandika zikiwa kwa kiulizi. | Mwanafunzi Tarakilishi<br><br>Kiswahili Dadisi Gradi ya tatu uk, 109-111 | |
| 14 | 1 | Mtihani. | | Wanafunzi wafanya mtihani. | | | | | |